HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE | TOLEO LA 005 | JANUARI 2023 | HALIUZWI

Jarida la

# TEMEKE YETU

FAHAMU ZAIDI



# "NITAKUWA BALOZI MZURI WA TEMEKE"

## -NAIBU KATIBU MKUU TAMISEMI

HABARI KAMILI UK. 2




## MEYA MTINIKA AKABIDHI VITI NA MEZA 100 KWA WALIMU TEMEKE

Mstahiki meya wa manispaa ya Temeke Mheshimiwa Abdallah Mtinika Januari 23, 2023 alikabidhi viti na meza 100 kwa walimu wa shule ya msingi Maji Matitu na shule ya sekondari Charambe vilivyotolewa na wadau wa maendeleo...

HABARI KAMILI UK. 3

## MHARIRI MKUU

**FRANCISCA MSELEMU**
Kaimu Mkuu - Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini
Manispaa ya Temeke

## WAHARIRI WASAIDIZI

**SHALUA MPANDA**
Afisa Habari - Manispaa ya Temeke

**NASSORO RASHID**
Afisa Habari - Manispaa ya Temeke

**SWEETBETTER NJIGE**
Afisa Habari - Manispaa ya Temeke

## WAPIGA PICHA

**MATHEW JONAS**

**VICTOR DEOGRATIUS**

## MSANIFU WA JARIDA

**MICHOLAX HARRY MUSSA**
Afisa TEHAMA - Manispaa ya Temeke

## JARIDA HILI HUTOLEWA NA;

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**
**S.L.P 46343 Temeke, DSM.**
**SIMU: +255 22-2928132**
**NUKUSHI: +255 22-2928137**
**BARUA PEPE: temeke@temekemc.go.tz**



# NITAKUWA BALOZI MZURI WA TEMEKE -NAIBU KATIBU MKUU TAMISEMI

Naibu katibu mkuu TAMISEMI ndugu Ramadhani Kailima Januari 4,2023 amefanya ziara ya kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za Sekondari, ambapo alitembelea pia ujenzi wa madarasa ya ghorofa katika shule ya sekondari Dovya na Lumo.

Akizungumza katika ziara hiyo Ndg. Kailima alisema amefurahishwa na utendaji kazi uliopo kwa watumishi na watendaji wa Temeke, alisema "Niwapongeze Temeke mnafanya kazi nzuri sana, Mkurugenzi na watendaji wako kazi inaonekana, umenileta hapa Dovya kuna ujenzi wa ghorofa  nne (04) yenye madarasa 32, lakini nilipita mwezi Novemba nikakuta madarasa 12 yanajengwa Mkurugenzi uliniahidi nikirudi yatakuwa yamekamilika nimekuta hivyo mimi nitakuwa balozi mzuri wa Temeke kwakuwa mnafanya mambo mazuri sana"

Aidha Ndg. Kailima amepongeza utaratibu ulioanzishwa na manispaa ya Temeke wa kuwafanyia "orientation" wanafunzi wa kidato cha kwanza waliochaguliwa kuanza masomo ya sekondari katika shule za sekondari za Kata husika,alieleza. "Niwapongeze Mkurugenzi,Madiwani na wakuu wa shule kwa utaratibu huu, mmefungua shule kwa kidato cha kwanza tu tangu Januari 02 na tayari 90% ya Wanafunzi wameripoti,hii sio tu inatusaidia kwenye takwimu lakini pia tunatengeneza mazingira watoto kuzoea mapema ikifika Januari 09, wanaanza kusoma moja kwa moja, nashauri Halmashauri nyingine ziige mfano huu, kwa shule za kutwa watoto wawe wanafanyiwa hivi".

Kwa upande wake Mkurugenzi wa manispaa ya Temeke amemshukuru Naibu Katibu Mkuu kwa kutembelea miradi hiyo na kuahidi kuendelea kupokea maagizo na kuyafanyia kazi.

Manispaa ya Temeke inatekeleza mradi wa ujenzi wa vyumba 207 vya madarasa katika shule mbalimbali za Sekondari,kadhalika kutokana na changamoto ya uhaba wa maeneo,Manispaa imeamua kujenga madarasa ya ghorofa ,ambapo utekelezaji wake umeanza katika shule ya Dovya na Lumo.




# MEYA MTINIKA AKABIDHI VITI NA MEZA 100 KWA WALIMU TEMEKE

Na **Sweetbetter Njige - TMC Habari.**

Mstahiki meya wa manispaa ya Temeke Mheshimiwa Abdallah Mtinika Januari 23, 2023 alikabidhi viti na meza 100 kwa walimu wa shule ya msingi Maji Matitu na shule ya sekondari Charambe vilivyotolewa na wadau wa maendeleo benki ya NMB.

Meya Mtinika ameipongeza benki ya NMB kwa kuiishi kauli mbiu yao "NMB Karibu yako" kwa kuwa karibu na Wanatemeke kwa kuendelea kufanya kazi na jamii kwa ukaribu mkubwa.

Aidha Mhe. Mtinika amewakumbusha Wanafunzi na Walimu wa shule hizo kusimama katika nafasi zao ili kuhakikisha nia na jitihada zinazofanywa na Serikali chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan katika sekta ya elimu inafanikiwa na kila Mtanzania anapata elimu bora.





# MKURUGENZI TEMEKE AKABIDHI VISHIKWAMBI

**Na: Sweetbetter Njige**

**Tmc habari.** Mkurugenzi manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya amekabidhi vishikwambi (Tablets) 6157 kwa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari pamoja na Maafisa Elimu ili kuwezesha katika shughuli zao za kila siku na hasa ufundishaji.

Akizungumza katika zoezi hilo la makabidhiano Januari 16 ,2023 Mkurugenzi Mabelya amewakumbusha na kuwataka walimu kuzingatia matumizi sahihi ya nyenzo hiyo na kufuata miongozo ili kuboresha ufundishaji na kuepuka kuitumia tofauti, alisema. "Vishikwambi hivi vimekuja kuboresha ufundishaji Temeke, visiende kutumika tofauti na maelekezo ya Serikali. Ninaamini ninyi wawakilishi wa walimu mtaenda kuwa mabalozi na mimi kama msimamizi mkuu ndani ya Halmashauri sitosita kuchukua hatua kwa watakaofanya matumizi tofauti na ambayo yametolewa kwenye muongozo". Alisema Mkurugenzi huyo

"Namshukuru Mheshimiwa Rais Dokta Samia Suluhu Hassan kwa kutujali Temeke na kujali elimu, ametupatia vishikwambi hivi ili kuboresha sekta ya elimu, vishikwambi hivi vikaboreshe ufundishaji na mbinu za ufundishaji, visiende kutumika tofauti"

- **Ndg. Elihuruma Mabelya,** Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke

Manispaa ya Temeke kama zilivyo manispaa nyingine Nchini imepokea vishikwambi kutoka Serikali kuu na kuvigawa kwa walimu, vishikwambi vilivyotolewa ni baaada ya kukamilika kwa matumizi ya zoezi la Sensa ya watu na makazi mwaka 2022.



# MKURUGENZI TEMEKE ATOLEA UFAFANUZI BOMOA BOMOA ENEO LA LUMO

Na **Nassoro Rashid - TMC Habari.** Mkurugenzi wa manispaa ya Temeke Ndugu Elihuruma Mabelya Disemba 12, 2022 ametolea ufafanuzi wa taarifa iliyotolewa kwenye moja ya chombo cha habari juu ya zoezi la ubomoaji wa vibanda vya makazi vya wananchi 56 eneo la Lumo wilayani Temeke.

Mkurugenzi Mabelya amesema zoezi hilo la ubomoaji limezingatia Sheria na Kanuni mara baada ya wananchi hao 56 kushindwa mashauri matatu mahakamani na kuamuliwa na Mahakama ya rufaa kuwa eneo hilo ni la Serikali na si la Wananchi hao. "Walifungua shauri mwaka 2000 lenye namba 140/2000 mahakama kuu wakidai kwamba eneo hili ni la kwao, na hitimisho lake walishindwa, wakafungua shauri lingine namba 80/2014 Mahakama ya rufaa na walishindwa tena, hawakuridhika walifungua tena shauri lingine mwaka 2019 lenye namba 116 na ukamilifu wa shauri hilo ulitupiliwa mbali Septemba 26, 2022 na Mahakama ya rufaa na kuhitimishwa kuwa eneo hilo ni la Serikali". Alisema Mkurugenzi Mabelya

Mkurugenzi Mabelya amesema wananchi hao wanapaswa kufahamu kwamba eneo hilo lina hati ya Serikali na amesisitiza wanafanya hivyo kwa sababu halmashauri ya manispaa ya Temeke ina uhitaji mkubwa sana wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya kimaendeleo. "Maelekezo ya Ofisi ya mkuu wa Mkoa pamoja na katibu tawala wa Mkoa ni kwamba maeneo yote tuhakikishe yanapimwa, na eneo hili limepimwa na tayari kazi za ujenzi wa madarasa zinaendelea, kwahyo niwaombe wananchi hawa wasije wakadanganywa, wakati mwingine uongo ukisemwa sana hubadilika unakuwa ukweli, hivyo lazima waamini kwamba eneo hili ni la Serikali na lipo chini ya mamlaka ya Mkurugenzi". Alisisitiza Mkurugenzi Mabelya.

Ifahamike kuwa jitihada hizi ni muendelezo wa kurasimisha maeneo yote ya Serikali yanayomilikiwa na halmashauri ya manispaa ya Temeke kwa kupimwa na kupatiwa hati ili yaendelezwe katika miradi ya elimu, afya, masoko na miundombinu mingine ya kimaendeleo.




# Lipa na Tozo kwa maendeleo ya Manispaa yetu.

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - Manispaa ya Temeke



# WAFANYAKAZI KIWANDA CHA NONDO MBAGALA WALIA NA MAZINGIRA MAGUMU YA KAZI

Na **Nassoro Rashid - TMC Habari.**

Baadhi ya wafanyakazi wa kiwanda cha kutengeneza nondo cha A.M Steel & Iron Mills kilichopo Mbagala wilayani Temeke wamelalamika kutokuwa na mazingira salama ya kufanyia kazi.

Wakizungumza na Mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya ambaye aliambatana na Mstahiki meya wa manispaa hii Mhe.Abdallah Mtinika wakati wa ziara ya kushtukiza walioifanya kiwandani hapo  Disemba 21,2022,wamesema mazingira wanayofanyia kazi ni hatarishi.

Mmoja wa wafanyakazi kiwandani hapo amewaeleza viongozi hao kuwa sehemu kubwa ya kazi zinazofanywa kiwandani hapo hutumia moto mkali lakini hawana vifaa vya kuwakinga na joto hilo kali hali inayoweza kuhatarisha afya zao.

Akizungumza mara baada ya kukagua kiwanda hicho,Mstahiki meya Mtinika ameonesha kusikitishwa na mazingira ya kazi katika kiwanda hicho na kuelekeza mamlaka husika kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa ili kuokoa maisha ya wafanyakazi hao.

" Leo tumekuja hapa baada ya kupata malalamiko ya muda mrefu,kwa kweli tuliyoyakuta ni mambo ya hatari,mazingira ya kazi si mazuri hata ukitazama wafanyakazi hawana vitendea kazi wanavaa kandambili,hii hali imenisikitisha".Alisema Mhe.Mtinika.

Naye mkurugenzi wa manispaa ya Temeke Elihuruma Mabelya amesema kiwanda hicho kimekiuka taratibu za uendeshaji huku akisisitiza kuwa Serikali inapenda uwekezaji kwa kuwa unawezesha kukusanya kodi lakini kodi hiyo isitoke kwenye mazingira yanayoumiza wananchi.

Mbali na mazingira yasiyo rafiki kwa wafanyakazi, Viongozi hao wamebaini uharibifu na uchafuzi wa Mazingira kiwandani hapo ambapo moshi unaotokana na shughuli za uzalishaji wa nondo umekuwa ukitoka nje na kuathiri wanaozunguka eneo hilo.

Licha ya kazi zinazofanyika kiwandani hapo kutumia kiwango kikubwa cha moto lakini wafanyakazi wa kiwanda hicho wamekutwa wakifanya kazi zao bila kuwa na kinga za mikono(gloves),viatu vigumu wala kofia ngumu.

Ziara hiyo ambayo iliwajumuisha wataalamu wa mazingira kutoka Manispaa ni matokeo ya kauli ya Mhe.Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ya kuwataka viongozi kwenda kutatua kero na changamoto za Wananchi.



# SIMAMIENI MIRADI KWA UADILIFU -MHE. NDEJEMBI

Na **Nassoro Rashid - TMC Habari.**

Kauli hiyo imetolewa Disemba 15,2022 na Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deogratius Ndejembi wakati akizungumza na watumishi wa manispaa ya Temeke katika ukumbi wa Idd Nyundo uliopo ofisi za Manispaa hiyo.

Mhe.Ndejembi amewataka watumishi wa Umma kufanya kazi na kutekeleza miradi inayoendelea katika halmashauri zote kwa kumtia nguvu Mhe Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uadilifu ili kuweza kumsaidia Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan "Watumishi wa Umma tutambue nafasi zetu na tujitume kwa kufanya kazi kwa moyo mmoja, lazima tuwe na miiko ya utumishi na kuyaishi maadili pamoja na kufanya kazi kwa mpangilio na sio kwa kufuata matukio." Alisema Mhe. Ndejembi

Aidha Naibu Waziri huyo amewataka watumishi kuwahudumia Wananchi vizuri huku akisisitiza kusimamia miradi ya Serikali kwa ukaribu ili kutimiza lengo la utawala bora na kuhakikisha kila mmoja kwa nafasi yake anasimamia miradi vizuri.

"Lazima tusimamie miradi ya Serikali kwa ukaribu sio mpaka aje Rais au Waziri Mkuu ndio ionekane dosari, yapo maeneo mengine usimamizi ni hafifu hivyo tushirikiane kila idara kusimamia kwa pamoja kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati kuendana na thamani ya fedha iliyotolewa". Alisisitiza Mhe.Ndejembi

Mhe. Naibu Waziri yupo katika ziarakatika Halmashauri mbalimbali nchini kusikiliza na kutatua changamoto mbalimbali za Watumishi wa Umma lengo ikiwa ni kukuza sekta ya menejimenti ya utumishi wa umma na utawala bora Tanzania.

**JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA**
OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**

# HATUA ZA KUKATA LESENI KWA MFUMO MPYA WA TAUSI

**Mfumo huu unapatikana kwenye anwani ya tovuti:**
**tausi.tamisemi.go.tz**

## 1. USAJLI (REGISTRATION)

- Namba ya NIDA (NIN)
- Namba ya simu iliyosajiliwa kwa namba ya NIDA
- E - Mail Address

## 2. MAOMBI YA LESENI (APPLICATION FOR LICENCE)

### A. MAOMBI BINAFSI

- TIN namba
- Mkataba wapango/ hati ya eneo
- Tax clearance

### B. KAMPUNI

- TIN namba
- Mkataba wa pango/ Hati ya eneo
- Tax clearance
- TIN namba ya mwakilishi wa kampuni (care taker)
- Memorundum
- Certificate of incorporatio
- Namba ya NIDA ya mwakilishiwa kampuni (care taker)

www.temekemc.go.tz







# MKURUGENZI TEMEKE AUNGANA NA JESHI LA POLISI KUMWAGA ZEGE LUMO SEKONDARI.

Na **Sweetbetter Njige - TMC Habari.**

Leo Januari 23,2023 mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya ameungana na jeshi la polisi mkoa wa kipolisi Temeke kumwaga zege ikiwa ni hatua za awali za ujenzi wa madarasa ya ghorofa yanayojengwa katika shule ya sekondari Lumo iliyopo katika kata ya Yombo Vituka.

Akizungumza katika zoezi hilo mkurugenzi Mabelya amelishukuru Jeshi hilo kwa kufanya maamuzi ya kushirikiana na jamii katika ujenzi wa madarasa hayo,alisema.

"Jeshi la polisi limetoa mchango wa nguvu kazi katika ujenzi wa madarasa haya.Tukio hili ni la kuigwa, sisi kama Halmashauri tumelipokea kwa mikono miwili, hii ni dhana ya kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa vitendo,hii ndio maana ya 'Kazi Iendelee'

Aidha mkurugenzi Mabelya ametoa wito kwa taasisi na mashirika mbalimbali kuunga mkono jitihada za Serikali kushiriki katika shughuli za kijamii hususani katika shughuli za kuboresha sekta ya elimu.

"Niombe mashirika na taasisi mbalimbali katika halmashauri yetu, kujitokeza kwa wingi kushiriki na kurudisha kwa jamii kwa kutoa sehemu ya faida yao au nguvu kazi ili kumuunga mkono mheshimiwa Rais hasa katika kipindi hiki anachojitoa kuwekeza katika sekta ya elimu, niwaombe tuige mfano huu uliooneshwa na Jeshi la polisi"

Kwa upande wake ACP John Malulu ameeleza furaha yake katika kushiriki zoezi hilo kama Maaskari na Wazazi.

"Tumekuja hapa kuunga mkono kazi nzuri ya Serikali yetu katika kuhakikisha watoto wa Temeke wanapata mahali pa kusoma, tutambue askari wa Temeke ni sehemu ya wana Temeke, tumeona ni muhimu kuja kuchangia nguvu kazi za mikono hapa kwakua watoto wakielimika watapata maarifa ya kufanya shughuli zao maalumu za kujitegemea na tutaondoa uhalifu"

Manispaa ya Temeke inatekeleza mradi wa vyumba 32 vya madarasa vinavyojengwa kwa mtindo wa ghorofa katika Shule ya Sekondari Lumo ambapo kwa sasa ujenzi upo katika hatua za mwanzo na unatarajiwa kukamilika mapema mwezi Machi,2023.



# MKUU WA MKOA WA DAR ES SALAAM AWAPONGEZA VIONGOZI TEMEKE

Na **Nassoro Rashid**
**TMC Habari.**

Mkuu wa mkoa wa Dar es salaam mheshimiwa Amos Makalla amefanya ziara ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya Mradi wa mabasi ya mwendokasi(BRT) awamu ya pili kuanzia eneo la Uhasibu mpaka Bandari huku akionesha kufurahishwa na viongozi wa manispaa ya Temeke katika usimamizi wa Mradi huo.

Akizungumza mara ya baada ukaguzi huo Januari 18, 2023 Mhe. Makalla aliwapongeza viongozi wa Temeke kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa barabara hizo awamu ya pili kwa kushirikiana vizuri na DART na TANROADS mpaka kufikia asilimia 82% hadi sasa.

"Nyie ni mashahidi nimekuja zaidi ya mara tatu hapa Temeke, Tumefanya jitihada kubwa mpaka kubadilisha wasimamizi ili huu mradi uende, na Temeke mkafanya mabadiliko na mkasimamia vizuri na Mkandarasi hatimaye tupo katika hali nzuri na kazi zinaonekana. Muendelee, na tuna hakika mpaka mwisho wa mwezi Machi mwaka huu mradi huu utakua umekamilika." Alisema Mhe. Makalla

Kadhalika Mhe. Makalla amempongeza Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kujengwa miradi ya kimkakati katika Mkoa wa Dar es salaam, awamu ya kwanza ikiwa imeshakamilika, na awamu ya pili ikiendelea vizuri.

Sambamba na hayo Mhe.Makalla amewataka wafanyabiashara wadogowadogo (Machinga) kuondoka barabarani na kurudi kwenye maeneo waliyopangiwa hususani eneo la Mbagala na maeneo mengine kwani ni maeneo hatarishi lakini pia kupisha ujenzi wa barabara hizo,ili uweze kukamilika kwa wakati.

# HALMASHAURI ZATAKIWA KUTENGA BAJETI YA KUTOSHA KUENDELEZA UMILIKISHWAJI ARDHI.



Na **Sweetbetter Njige - TMC Habari.**

Kauli hiyo imetolewa Disemba 17, 2022 na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Mhe. Angelina Mabula wakati akiendesha zoezi la utoaji wa hati za ardhi lililosimamiwa na ofisi ya Kamishna Msaidizi wa ardhi Mkoa wa Dar es salaam kwa kushirikiana na halmashauri ya manispaa ya Temeke lililofanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Mbagala Kuu wilayani humo.

Akiongea na Wananchi Mhe. Mabula amesema lengo la kuwasogezea huduma hiyo karibu ni kuweza kuwaimarisha na kuwawezesha kupata nyaraka sahihi na uhakika wa usalama wa miliki zao huku akiwasisitizia kuhakikisha kabla ya mwaka huu kuisha wawe wamerasimisha "Mhe. Rais ameelekeza tuhakikishe kabla ya muda kuisha, wale wote wanaohitaji kufanyiwa urasimishaji wafanyiwe na hii ndo tunakwenda nayo kwa kasi, kwa mkoa wa Dar es Salaam na Halmashauri zake zote tano, idadi ya viwanja vilivyotambuliwa kwa ajili ya urasimishaji ni 610,689 kwa wilaya zote, michoro 2084 imeidhinishwa na viwanja 549,387 vimepangwa na vimeidhinishwa tayari kwa umilikishaji". Alisema Mhe. Mabula

Sambamba na hayo Mhe. Mabula amesema mpaka sasa umilikishaji umefanyika huku hati zilizoandaliwa ni 24689 kati ya viwanja vilivyoidhinishwa 549,387 kwa Mkoa wa Dar es salaam na kuwataka wananchi kutumia fursa hiyo ili kupata hati zao kadhalika ametoa maelekezo mbalimbali kwa viongozi wa Halmashauri na ofisi ya Kamishna Msaidizi.

"Hakikisheni Halmashauri mnatenga bajeti za kutosha kuweza kuendeleza zoezi la umilikishaji na upangaji katika maeneo yenu, naelekeza uandaaji wa hati kwa haraka kulingana na maombi yaliyokamilishwa, naelekeza ndani ya siku 14 kuhakikisha mnayafanyia kazi maombi ya hati na kuwapatia wananchi, naelekeza hakuna kutoa hati yoyote kwa mkono kama tulivyokuwa tunatoa zamani".
Alisema Mhe. Mabula

Kadhalika Mhe.Waziri Mabula ameelekeza kabla ya mwaka huu kuisha makampuni yote ya urasimishaji ndani ya jiji la Dar es salaam chini ya usimamizi wa Kamishna Msaidizi kukaa kikao kazi pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri zote ili kuja na mikakati mahsusi ya kukwamua zoezi hilo.





# TEMEKE SAFI

*Inawezekana!*



# KAMATI YA FEDHA TEMEKE YAMPONGEZA RAIS SAMIA

Na **Sweetbetter Njige - TMC Habari.**

Januari 11,2023 kamati ya fedha na Uongozi Manispaa ya Temeke ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa katika Manispaa hii ili kukagua miradi hiyo.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo mbunge wa jimbo la Temeke Mheshimiwa Dorothy Kilave amemshukuru Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania na kupongeza jitihada za Serikali kwa nguvu kubwa iliyowekezwa katika sekta ya elimu hususani kwa wilaya ya Temeke, alisema

"Nampomgeza sana Mhe. Rais kwa hakika amefanya kazi kubwa sana kwa fedha alizotuletea, hapa Lumo tuna jumla ya vyumba 58 kati ya hivyo vyumba 32 ni vya mradi wa ghorofa na 26 ni madarasa msambao, hii inaonesha kwa namna gani mama ameamua kujikita katika elimu, sisi kama wana Temeke na wazazi wa Temeke tunamshukuru sana, tumeona pia katika shule hii (Lumo) Wanafunzi 445 wa kidato cha kwanza wamepokelewa na wote wameingia darasani"

Kwa upande wake diwani wa kata ya Yombo Vituka Mhe. Fulgence Rwiza ameshukuru jitihada za Serikali kupitia kampeni maarufu ya "KAPU LA MAMA" kwa kuipatia kata yake madarasa 58 ambayo kwa kiasi kikubwa yataondoa kero kwa wazazi kutafuta shule katika kata jirani kwa ajili ya watoto wao.

"Leo tumekuta Wanafunzi wameingia madarasani katika vyumba vilivyowezeshwa na Mhe. Rais kupitia Kapu la mama, nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Rais kwa kuonesha kiasi gani anawajali Watanzania, ni namna gani anawajali kina mama na watoto, ukimsaidia mtoto unakuwa umemsaidia mama, kutusogezea shule na vyumba vya madarasana ni kumsaidia mama, niwaombe Wananchi tuitunze miradi hii"

Manispaa ya Temeke inatekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kuhakikisha Wananchi wanapata huduma bora na katika mazingira bora.



# RC MAKALLA:ACHENI KUPANGA BIASHARA BARABARANI.

Na **Shalua Mpanda - TMC Habari.** Mkuu wa mkoa wa Dar es salaam mheshimiwa Amos Makalla amewataka wafanyabiashara wanaofanya biashara maeneo yasiyoruhusiwa hasa ya barabara kuondoka maeneo hayo ili kuweza kutunza miundombinu hiyo.

Mhe.Makalla amesema hayo leo Januari 28,2023 wakati wa kampeni maalum ya usafi ya kila mwisho wa mwezi ambayo Kimkoa imefanyika katika kata ya Charambe, mtaa wa Rangitatu.

"Barabara za mabasi ya mwendokasi ni maalum kwa mabasi hayo na si kwa ajili ya kupanga biashara,waulizeni wenzenu wa Msimbazi walikuwa wanapanga biashara kwenye barabara hizo,kila siku walikuwa wanagongwa na mabasi hayo".Alisema Mkuu huyo wa Mkoa.

Aidha Mhe. Makalla amewataka Wafanyabiashara hao kuacha kufanya biashara katika barabarani hiyo ili kumuwezesha Mkandarasi kufanya kazi zake kwa uhuru.

Awali akiongea na Wananchi waliojitokeza kufanya usafi katika eneo hilo Mkuu huyo wa Mkoa aliwataka Wananchi hao kujenga tabia ya kufanya usafi kwenye maeneo yao na sio kusubiri mwisho wa mwezi, huku akisisitiza pia upandaji wa miti na utengenezaji wa bustani kwenye makazi yao ili kuifanya Dar es Salaam kuwa ya kijani.

Akimshukuru Mkuu wa mkoa,Mstahiki meya wa manispaa ya Temeke Mhe. Abdallah Mtinika amesema mkuu wa mkoa wa Dar es salaam amekuwa ni kiongozi anayeonesha kwa vitendo kuwa ni mtu anayependa usafi ambapo katika kudhihirisha hilo aliandaa ziara ya viongozi wa mkoa wa Dar es salaam kwenda nchini Rwanda kujifunza namna ya utunzaji wa mazingira.

Kampeni ya usafi wa kila mwisho wa mwezi ambayo ilianzishwa na Mkuu huyo wa mkoa,imekuwa na mafanikio makubwa ambapo imesaidia kupunguza magonjwa ya mlipuko hasa kipindupindu kilichokuwa kinasumbua katika Mkoa huu.




# MKURUGENZI TEMEKE ASISITIZA MABORESHO UJENZI UWANJA WA MWEMBEYANGA.

Na **Sweetbetter Njige - TMC Habari.** Timu ya menejimenti ya Manispaa ya Temeke ikiongozwa na Mkurugenzi wa Manispaa ndugu Elihuruma Mabelya imetembelea uwanja wa Mwembeyanga ili kukagua maendeleo ya ujenzi wa uwanja huo unaotekelezwa na Serikali kupitia mradi wa DMDP.

Katika Ukaguzi huo timu hiyo ilibaini mapungufu kadhaa ambapo Mkurugenzi Mabelya alimtaka mhandishi mshauri wa mradi huo Mhandisi Selemani Hamduni kuhakikisha kwamba marekebisho yanafanyika mara moja ili ujenzi huo uendane na thamani ya fedha iliyotumika, vinginevyo hatua za kisheria zita chukuliwa dhidi yake.

Akizungumza wakati wa Ukaguzi huo Mkurugenzi Mabelya alisema...

" Sijaridhishwa na kazi iliyofanyika hapa, thamani ya fedha iliyotumika haionekani hapa.Fedha iliyotumika hapa ni ya Serikali,lazima thamani ya kinachojengwa ilingane na fedha inayotumika.Maelekezo yangu ni haya, mapungufu yote tuliyoyainisha yafanyiwe kazi haraka kabla mradi haujakabidhiwa."

Akijibu kuhusu mapungufu hayo Mhandisi Hamduni aliahidi kufanya marekebisho ,na baada ya kukamilisha ataiomba timu hiyo ya Menejimenti kufika na kufanya tena ukaguzi .

Eneo hilo la Mwembeyanga limeingia katika sura hiyo mpya ya maboresho kwa madhumuni ya kupendezesha mandhari yake na kuwezesha Wananchi kuwa na mazingira bora ya michezo kwa kuzingatia upatikanaji wa viwanja vya mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa pete, mpira wa wavu, eneo la mchezo wa ngumi pamoja na maeneo ya kupumzikia.

# JAMII YATAKIWA KUFICHUA VITENDO VYA UKATILI WA KIJINSIA

Na **Shalua Mpanda - TMC Habari.**

Ikiwa Dunia inaadhimisha siku 16 za kuhamasisha mapambano dhidi ya ukatili kwa Wanawake na Watoto,Jamii imetakiwa kutokufumbia macho vitendo hivyo vya unyanyasaji.

Wito huo umetolewa na Mrakibu Mwandamizi wa Polisi mkoa wa kipolisi Chang'ombe SSP Ariziki Makwaya wakati akizungumza na wakazi wa kata ya Kurasini Novemba 30,2022.

Amesema kuwa matukio mengi ya kikatili na unyanyasaji yanatokea kwenye jamii na mara nyingi yamekuwa yakifichwa kutokana na mahusiano ya karibu na wanaotekeleza matukio hayo. "Jeshi la Polisi linatekeleza majukumu yake ya ulinzi na usalama,na hatuwezi kutenganisha suala la usalama na haki ya kuishi ambayo imezungumzwa kwenye katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania".Alisema SSP Makwaya.

Aidha amewataka wanafunzi wenye tabia zisizo na maadili kuacha tabia hizo, badala yake wajikite katika masomo kwa kuwa kwa kufanya vitendo hivyo watajiingiza kwenye mikono ya sheria.

Diwani wa viti maalum mheshimiwa Caroline Henrich ambaye alikuwa ni mmoja wa waalikwa katika maadhimisho hayo amewaasa wazazi kuwa karibu na watoto wao na kujenga tabia ya kuwa marafiki ili waweze kutambua changamoto wanazokutana nazo.

Maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wanawake na watoto yanafanyika kila mwaka,ili kuikumbusha Jamii kukemea vitendo hivi.




HALMASHAURI
YA MANISPAA YA TEMEKE
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
UNGANA NASI SASA KWENYE MITANDAO YA KIJAMII
Kupitia akaunti zifuatazo
instagram/ temeke_mc
facebook/ temeke mc
twitter/ temekemc
youtube/ tmc tv
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
www.temekemc.go.tz

Jarida hili limeandaliwa na;

Kitengo cha Mawasiliano Serikali

**MANISPAA YA TEMEKE**